## 4.2 KISWAHILI (102)

### 4.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

**1.** Hii ni hotuba. Vipengele viwili vikuu vya utungo wa aina hii; Maudhui na muundo vizingatiwe.

(a) **Muundo**

Vipengele vifuatavyo vya kimuundo vijitokeze:

(i) **Utangulizi** ambapo mtahiniwa atataja waliohudhuria kwa vyeo kulingana na hadhi. Pia kiini cha hotuba kishughulikiwe hapa.

(ii) **Mwili** - yaliyomo yajadiliwe na yatolewe ufafanuzi.

(iii) **Hitimisho** - ionyeshe msimamo wa hatibu kuhusiana na suala la ushauri - nasaha. Aidha, atoe shukrani kwa hadhira yake na kuiaga.

(b) **Maudhui**

Mtahiniwa afafanue hoja zinazoonyesha haja ya kuwepo na ushauri - nasaha shuleni. Baadhi ni:

(i) Huwasaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto za kuzoea mazingira ya shuleni hasa endapo mazingira yale ni mageni. Hawa huelekezwa kuhusu namna ya kukubali na kufuata sheria za shule ili wasijihisi kuwa wananyanyaswa

(ii) Kushindwa kufikia shabaha alizojiwekea au alizowekewa huwafanya baadhi kuvunjika moyo na kukata tamaa, kabla hawajakata tamaa na kufanya uamuzi usiofaa, wanafunzi hawa wanahitaji msaada wa ushauri - nasaha.

(iii) Wanafunzi kama wanajamii wengine, huweza kutatizika kihisia na kifikira, na wakati mwingine huchoshwa na maisha. Ni muhimu huwapa huduma za ushauri nasaha ili kuwaandaa kujidhibiti, na kukabiliana na hali hizi.

(iv) Wanafunzi wengi, hasa wanaobaleghe hukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya mwili katika kukua kwao. Wengine huingiwa wa wasiwasi kufedheheka, au kuhuzunika kutokana na hali hizi. Huduma za ushauri nasaha zitawasaidia sana kukabiliana na hali hizi kwa njia chanya.

(v) Huwasaidia wanafunzi kukabiliana na shinikizo la marika, na shinikizo kutoka kwa wazazi na wanajamii wengine.

(vi) Wanafunzi waliotatizika kiakili na ambao hawawezi wakatatua migogoro inayowakabili kwa njia salama na chanya huwa na ushawishi mkubwa kwa wengine na wasiposaidiwa kwa ushauri nasaha, wanaweza kuwapotosha wengine.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(vii) Huwaelekeza vijana kuhusu namna ya kufaidika kwa njia za kisasa za mawasiliano bila kupotoshwa na tamaduni za kigeni zinazoandamana nazo.

(viii) Ushauri nasaha huisaidia shule kudumisha nidhamu miongoni mwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi.

(ix) Wanafunzi huhitaji kuelekezwa kuhusu namna ya kuuratibu muda wao shuleni.

(x) Ushauri nasaha huwasaidia wazazi kukabiliana na adha za malezi. Mzazi aliye na matatizo ya kuhusiana vyema na mwanawe anaweza kushauriwa kuhusu jinsi ya kumwelewa mwanawe.

(ix) Huelekeza wanafunzi kuhusu taaluma au kozi wanazoweza kuchagua baada ya kuhitimu masomo yao.

(x) Humwelekeza mwalimu kuhusu namna ya kuhusiana na wanafunzi.

(xi) Ni njia ya kuwasaidia walimu na wanafunzi kukabiliana na majanga kama vile vifo, magonjwa hatari, na kufutwa kazi.

(xii) Ushauri nasaha, hasa ushauri marika, huwasaidia wafunzi ambao wanawiwa vigumu kuwatolea wazazi au walezi undani wao, kuwaambia wanafunzi wenzao hivyo kusaidiwa.

**Tanbihi**

(i) Katika utangulizi, mtahiniwa lazima aonyeshe uelewa wa hadhira, awataje kwa mfuatano ufaao kulingana na vyeo.

(ii) Muktadha wa hotuba unaweza kuwa:

- (a) siku ya kuwatuza wanafunzi bora shuleni,
- (b) siku maalum ya kuwaaga wanafunzi wa kidato cha nne,
- (c) siku ya kuwaelimisha wazazi na jamii nzima ya shule kuhusu umuhimu wa ushauri - nasaha; pengine ili kamati ya wazazi iidhinishe kuajiriwa wa afisa wa utuoji nasaha.

(iii) Mtahiniwa anaweza kutoa hotuba kuhusu jinsi alivyofaidika kwa ushauri nasaha katika kipindi cha miaka minne aliyokuwa shuleni, bora tu yasiwe masimulizi bali mazungumzo ya moja kwa moja kwa hadhira lengwa.

(iv) Anaweza pia kutoa hotuba, pengine kukashifu mielekeo hasi ya wazazi na wanafunzi kuhusu udumishaji wa nidhamu, akaonyesha kwamba tabia ya binadamu huimarishwa zaidi kupitia ushauri - nasaha kuliko matumizi ya nguvu au adhabu kali.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(v) Katika kutathmini, kumbuka kwamba mwanafunzi anaweza kutumia maswali ya balagha ili kuchochea hisia fulani, au kukashifu mwelekeo fulani. Huu unaweza kuhesabiwa kama upekee unaomtofautisha mtahiniwa na wengine wa kiwango cha chini.

(vi) Mtindo wa uwasilishaji wa hotuba uzingatiwe. Hatibu azungumze moja kwa moja na hadhira yake. Asitumie mtindo wa masimulizi ila pale tu, pengine anapotoa kisa kifupi kama kielelezo cha mtu aliyefaidika kwa ushauri-nasaha, au mzazi aliyehasirika kwa kutotumia ushauri-nasaha katika malezi.

**2.** Hii ni insha ya maoni. Inaweza pia kuwa insha ya maelezo. Vipengele vikuu vya insha ya aina hii: Muundo, maudhui vizingatiwe:

(a) **Muundo**

Vipengele vifuatavyo vizingatiwe:

(a) **Utangulizi** - uangazie hali ya matumizi ya ardhi nchini.

(b) **Mwili**

Hapa ndipo yaliyomo / maudhui yanapojadiliwa. Mtahiniwa:

(i) Ajadili hoja ambazo zinadhihirisha namna ambavyo rasilimali za nchi (zinazohusiana na ardhi) zinavyotumiwa vibaya huku akionyesha athari mbaya za hulka hizi.

(ii) Aonyeshe mchango wa raia katika uharibifu wa mazingira au matumizi mabaya ya ardhi.

(c) **Hitimisho**

Mtahiniwa:

(i) Ajumuishe hoja alizojadili na kuonyesha mwelekeo, msimamo au falsafa yake kuhusiana na matumizi ya ardhi.

(ii) Anaweza kutoa wito kwa raia kuepuka mazoea ya kutumia ardhi vibaya.

(iii) Anaweza pia kupendekeza njia bora za kutumia ardhi kwa njia endelevu.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(b) **Maudhui**

Baadhi ya hoja ni:

(i) kulima kandokando ya mito, hivyo kusababisha mmomonyoko wa udongo

(ii) kupanda zao hilo hilo, hivyo kupujua (kudhoofisha) uwezo wa udongo kuzalisha mazao bora

(iii) ardhi ambayo imetengewa kilimo kutumiwa kwa ujenzi, hivyo kusababisha kutojitosheleza kwa chakula

(iv) kufuga mifugo wengi ambao wanaishia kufa wakati wa ukame, au kusababisha mmomonyoko wa udongo

(v) kutotumia sehemu zenye vinamasi kwa njia endelevu, badala yake wanajenga huko na kusababisha hata kuporomoka kwa majengo

(vi) kunyakua ardhi na kutenga katika sehemu zilizotengewa matumizi maalum kama vile maziara namadhabahu

(vii) wakulima kutumia kemikali ambazo zinaishia kuua wadudu ambao huchangia kuboresha udongo

(viii) wenye viwanda kuelekeza taka zenye kemikali kwenye mashamba na mito na kusababisha vifo vya wanyama na kuharibika kwa mimea

(ix) kufyeka misitu kwa ajili ya majengo na kasababisha kuenea kwa jangwa au kupalilia ukame

(x) uwindaji wa wanyama ambao unatishia kupunguza aina za wamyama kama vile ndovu na kifaru

(xi) kujenga kwenye sehemu zilizotengewa ujenzi wa barabara hivyo kuathiri ustawishaji wa miundomsingi

(xii) kujenga majengo mengi kwenye sehemu ndogo ya ardhi, hivyo kusababisha kusongamana kwa watu

(xiii) Wawindaji haramu kuchimba vidimbwi vya kuwatilia wanyama sumu. Hili linasababisha vifo vya wanyama na kuzagaa ovyo kwa mizogo. Binadamu wanaweza pia kuumia kwa kutumbukia kwenye vidimbwi hivi

(ix) binadamu kukata miti kwa ajili ya samani na nishati, kutopanda mingine, na kusababisha kukosekana kwa aina muhimu za miti.



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

**Tanbihi**

Suala la matumizi mabaya ya ardhi liangaziwa katika upana wake. Mtahiniwa asitarajiwe tu kuzungumzia kilimo, anaweza kujadili aina nyingine za matumizi mabaya ya ardhi au mazingira.

**3.** Hii ni insha ya methali.

Mtahiniwa abuni kisa kinachodhihirisha maana ifuatayo:

Mtu anayetia bidii katika jambo gumu huja kupata faida, hata kama faida hiyo ni kidogo. Kisa kinaweza kudhihirisha hali zifuatazo:

(i) Mhusika, kama vile mwanafunzi, aliyejikuta katika mazingira magumu (kwa mfano kusoma, licha ya kufukuziwa karo), akajibidiisha, asikate tamaa, na hatimaye akaja kufaidika.

(ii) Mhusika anayejaribu kwa hali na mali kubadilisha mitazamo hasi ya wanakijiji, na kuinua hali zao za maisha na baadaye kufanikiwa.

(iii) Mhusika aliyepata pingamizi nyingi kazini, akataka kukata tamaa na kujiuzulu, lakini akajiasa au akaaswa na mwingine, akaamua kufanya kazi kwa ustahimilivu, na hatimaye juhudi zake zikatambuliwa, akapandishwa cheo.

(iv) Mhusika kijana aliyehitimu chuoni, akatafuta kazi ya ajira asipate. Baadaye apate mtaji wa kuanzishia biashara ndogo (pengine kupitia Hazina ya Uwezo), apate changamoto nyingi mwanzoni, lakini ajikakamue. Hatimaye mradi wake ufanikiwe, aweze hata kubuni nafasi za kazi kwa vijana wenzake.

(v) Mhusika anaweza kuwa mwenye mahitaji maalum yanayomzuia kujiendeleza, kwa mfano, asiwe na mikono, lakini ajibidiishe, asiuone ulemavu kama kikwazo, na mwishowe kufanikiwa.

(vi) Mzazi au mlezi anaweza kuwa na mtoto aliyepotoka, ajaribu kumrekebisha na baadaye mtoto huyu abadilike na hata kumfaa mzazi au jamii pana.

**Tanbihi**

(i) Kwa vyovyote vile, **lazima** kuchanika (kujibidiisha, kuteseka) kujitokeze. Mhusika aonekane akikabiliana na kizingiti fulani, pengine cha kimaumbile au kinachotokana na mazingira anamoishi.

(ii) Katika kuchanika huku, tuone juhudi anazotumia kukabiliana na vikwazo vinavyomkabili.

(iii) Hatimaye **sharti** faida ijitokeze. Hapa tunaweza kuona manufaa ya kazi aliyofanya, au namna alivyojitoa kwenye hali ngumu iliyomkabili.



Powered by: www.manyamfranchise.com

MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

**4.** Hii ni insha ya mdokezo inayomhitaji mtahiniwa kuyasanisi mawazo yake na kubuni hadithi inayoafikiana na mwanzo huu.

Mdokezo unafumbata hali zifuatazo:

a. Msimulizi anaondoka katika mazingira aliyozoea (kuvuka kizingiti cha lango).

b. Msimulizi anaanza safari fulani / anaingia katika hali nyingine (maisha kuchukua mkondo mpya).

c. Msimulizi ana hakika kuwa mustakabali wa maisha yake umebadilika (nilijua).

Kisa kinaweza kudhihirisha hali kama vile:

(i) Msimulizi amepita mtihani wa darasa la nane na anaelekea shule ya upili ambamo anatarajia maisha yake kuwa tofauti. Aonyeshe mkondo huo mpya wa maisha yake.

(ii) Msimulizi amekuwa mjane au mseja kwa muda, ni siku yake ya arusi, anatarajia maisha mapya ya ndoa.

(iii) Msimulizi amehitimu masomo ya kidato cha nne, amepata fursa ya kwenda ng'ambo kwa masomo ya chuo kikuu, anajua kuwa maisha yatakuwa tofauti. Anaweza pia kusimulia maisha yake huko ng'ambo ili kuonyesha mabadiliko haya.

(iv) Msimulizi amepata kazi ya ajira anaondoka kwao alikozoea na kutarajia mabadiliko.

(v) Msimulizi, baada ya kauli hii, anaweza kuturudisha nyuma, akatumia mbinu rejeshi kuonyesha hali ya maisha yake hapo awali, pengine amekuwa akiishi kwenye mazingira yenye udhalimu, kisha akafikia uamuzi wa kujinasua kwa kuondoka humu.

(vi) Msimulizi anaweza pia, baada ya kauli hii, asiturejeshe nyuma, asimulie kisa chake moja kwa moja. aonyeshe namna alivyokuwa ameingojea siku hii kwa hamu, asimulie kuhusu safari yake, adha, furaha ya safari hii hadi anapofika alikoondoka kwenda.

(vii) Msimulizi anaweza kuwa kijana mtoro ambaye anayaona maisha ya kwao nyumbani kuwa ya kudhibitiwa. Aamue kuondoka kwao. Hapa tunatarajia msimulizi asimulie, ama maisha yake ya awali, au aonyeshe namna alivyosafiri, na namna hali haikuwa alivyotarajia pengine hapati uhuru aliotarajia, aadhibiwe kwa utoro wake.

(viii) Anaweza pia kuwa mwanariadha mashuhuri anayeondoka kwao kwa kinyang'anyiro, pengine mbio, kisha asimulie kuhusu shindano, na jinsi alivyoimbuka mshindi, akapata pato kubwa na kutoka kwenye hali ya umaskini.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

**Tanbihi**

(i) Mdokezo unaelekeza kwamba kisa kitasimuliwa kwa nafsi ya kwanza.

(ii) Hata hivyo, kwa vile msimulizi huenda akakumbana na wahusika wengine, anaweza pia kuchanganya nafsi ya kwanza na ya pili.

(iii) Mazungumzo au dayolojia za wahusika zinaweza kujitokeza kulingana na ukomavu wa lugha ya mtahiniwa.

(iv) Si lazima mtahiniwa ataje mkondo mpya moja kwa moja.

(v) Si lazima afafanue mabadiliko kwa mapana na marefu. Mtahini atambue mabadiliko yanayojitokeza kisha amkadirie mtahiniwa kwa mujibu wa mwongozo wa kudumu.



Powered by: www.manyamfranchise.com

MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

### 4.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

1. (a)

(i) kutengwa na mazingira ya nyumbani
(ii) kudhulimiwa mali na jamaa za wazazi
(iii) ajira ya watoto - Duma kutumikishwa shambani
(iv) kudidimizwa katika ulanguzi wa dawa
(v) kusababishiwa uraibu wa dawa
(vi) wasiwasi - Duma akiwa mchanga kujazwa wasiwasi / woga
(vii) badala ya mwajiri kumwonea Duma imani, anamshutumu kwa kushikwa
(viii) kuhatarishiwa afya kwa kuhitajika kuzimeza dawa ili kuzisafirisha ughaibuni
(ix) kukatiziwa malezi - anatolewa nyumbani akiwa mchanga / kabla ya ubwabwa wa shingo kumtoka
(x) kuumbuliwa kwa moyo utu /kufanywa kuwa na moyo mgumu /usugu / ugumu wa moyo
(xi) kusababisha matumizi ya dawa shuleni.
(xii) kumfanya kuwa mvunja sheria / kumhusisha katika ufisadi.

5 x 1 = 5

(b)

(i) **Magonjwa** - wazazi wa Duma wanatumia pesa nyingi kwenye matibabu; wanamwacha mnyonge hivyo kuwa windo rahisi la uraibu na ulanguzi wa dawa.
(ii) **Uyatima** - Duma anakosa walezi hivyo kutoswa kwenye ulanguzi.
(iii) **Tamaa** - jamaa za Duma wanampoka mali kutokana na tamaa. Duma anaingilia ulanguzi wa dawa kwa sababu ya tamaa.
(iv) **Ufisadi** - maafisa wa usalama wanapokea hongo na kuendeleza ulanguzi wa dawa zaidi.
(v) **Uraibu wa dawa za kulevya** unamfanya Duma kutojidhibiti, anaendelea kuzitumia na kuzilangua kwa kupata nguvu mpya / msukumo.
(vi) **Utoto/umri mbichi** - unamfanya Duma kuwa windo Jepesi la mjomba Duma.
(vi) **Umaskini**
(vii) **Marafiki/walimu** - kumfunza Duma matumizi ya dawa.

4 x 1 = 4

(c)

(i) Duma anakubali kuziuza dawa shuleni na sokoni.
(ii) Duma anajaribisha kutumia dawa hadi kuwa mraibu sugu.
(iii) Badala ya kuwajibika kubadilika Duma anajiona kuwa mtendwa.
(iv) Anakubali kumeza dawa ili kuzisafirisha.
(v) Duma anahalalisha matendo yake, hivyo kutoyarekebisha.



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(vi) Duma anawahonga polisi aachiliwe, hivyo kudidimia zaidi katika maovu.
(vii) Anashirikiana na mwajiri wake ili kuzua mbinu mpya za kuendeleza uhalifu; anakosa tahadhari na kuishia kukamatwa.
(viii) Hata anapojiwa na wazo la kubadilika hatuoni akilifuatilia; analiahirisha.
(ix) Tamaa inamfanya asingatuke kutoka kwenye uhalifu.

4 x 1 = 4

**Tanbihi**

Baadhi ya watahiniwa wanaweza kujadili pande zote mbili wakatoa baadhi ya hoja za kupinga kama vile:

(i) Duma anaingizwa kwenye biashara hii na watu waliomzidi ki-umri - mjomba Papa.
(ii) Kupokwa kwa mali kulimfanya kutafuta mbinu za kujikimu.
Hata hivyo, kwa vile swali linamhitaji kuthibitisha kauli hii, hoja za kuunga zichukue alama zaidi (alama 3), alama ya kupinga iwe moja (1).

(d)
(i) Wenye makini / waangalifu / walio macho kupambana na wahalifu
(ii) Ndizo zinazomwendeshea maisha / amekuwa mraibu sugu /ndizo zinazompa msukumo wa kuendelea na uhalifu.

2. (a)
(i) Suala la kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula linahitaji kushughulikiwa kwa dharura
(ii) Kila binadamu anahitaji kupata chakula chenye virutubishi.
(iii) Serikali inapambana na tatizo la chakula kwa kutoa misaada
(iv) Wakati wa kiangazi wahitaji hasa hufa kutokana na njaa
(v) Kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi wa chakula husababisha ukosefu wa chakula.
(vi) Ukosefu wa maji huzikumba sehemu kame kutokana na uhaba wa mvua.
(vii) Ukosefu wa mvua huzua hali ya utegemezi.
(viii) Wengine hula hata visivyostahili kuliwa.
(ix) Mbinu hasi za ukulima huathiri utoaji wa mazao.
(x) Wakulima wengine hupalilia mmomonyoko wa udongo kwa kulima kando ya mito, kulima eneo lilelile na kutopanda mimea inayozuia mmomonyoko wa udongo.
(xi) Baadhi ya wakulima kutopanda mimea inayostahimili ukame
(xii) Wafugaji kufuga mifugo wengi wasiostahimili ukame na kusababisha vifo
(xiii) Watu kutojua umuhimu wa lishe bora

8 x 1 = 8
mtiririko - 1


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(b)

(i) Serikali imechimba visima na mabwawa katika sehemu kame ili kunyunyizia mashamba maji.

(ii) Wakulima kupanda mimea ya kuatika inayokomaa haraka ili kukabiliana na njaa.

(iii) Kufuga kuku wa kututumuliwa wanaoweza kuuzwa na kununua aina nyingine ya chakula.

(iv) Wakulima kuhimizwa kutumia njia za kisasa za uzalishaji na uhifadhi wa chakula.

(v) Wakulima wadogowadogo wakome kuuza vyakula vyao kiholela .

(vi) Wanaoishi kwenye vinamasi wavitunze na kuvitumia kwa njia endelevu.

(vii) Vijana washauriwe kushughulikia kilimo mashambani.

(viii) Waishio mijini watumie visehemu wanavyopata kuendeleza kilimo cha bustani.

5 x 1 = 5
mtiririko - 1
Jumla - 6
**Au 6 x 1 = 6**

4. (a)

(i) Silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. **mf nda - ma** ; katika : ndama

(alama 2)

**Au**

Ni sauti moja au zaidi zinazotamkwa kama fungu moja la sauti / kama sauti moja.
Mf. o - a katika oa

2/0 - (alama 2)

(ii)

| | | |
|---|---|---|
| afya | enda | upwa |
| anza | anga | igwa |
| ibra | uzwa | |

1 x 1 = (alama 1)

(b) yu - kitenzi kishirikishi / kishirikishi kipungufu
anajaribu - kitenzi kisaidizi
kujinasua - kitenzi kikuu

3 x 1 = (alama 3)

(c) Mpira haukuchezeka kwa sababu ya mvua nyingi.

au

Mpira haukuchezwa na wachezaji kwa sababu ya mvua nyingi.

2/0 - (alama 2)

(d) Dobi atakuwa amewapigia watu nguo pasi. 2/0 - (alama 2)


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(e) **Udhaifu** wa kazi zao **<u>ulifichuka</u>** **<u>kabla ya</u>** **<u>kusitishwa</u>** kwa mradi ule.

(Kumalizwa)
(Kukamilishwa)
(Kuhitimishwa)
(Kukomeshwa)

($\frac{1}{2}$ x 4 = alama 2)

(f) (i) Kirai ni fungu la maneno ambalo hudokeza maana lakini maana hiyo si kamili.

**au**

Kirai ni fungu la maneno ambalo huainishwa kwa kuzingatia neno lake kuu. Kwa mfano, nomino ndilo neno kuu la kirai nomino.

(ii) (a) na mafundi - kirai husishi/kirai kihusishi.

(alama 2)


(b) wenye ustadi mkubwa - kirai kivumishi / kirai vumishi

(alama 1)
2x $\frac{1}{2}$ = 1


(g) Kinga ni jambo au dawa ya kujiepusha na madhara.
Kinga ni kipande cha ukuni chenye moto.
Kukinga ni kutayarisha bindo, mkono au chombo ili kupokea kitu.

(1 x 2 = alama 2)

(h)




au




(8 x $\frac{1}{4}$ = alama 2)



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(i) (i) Wakimbizi ndio wanatamani.
(ii) Watu wengine wanatamani.
(iii) Wakimbizi watarudi nyumbani kwa wakimbizi.
(iv) Watu wengine watarudi kwao (hao wengine).
(v) Watu wengine watarudi kwa wakimbizi.

(2 x 1 = alama 2)

(j) dh + kikwamizwa / kikwaruzo
+ ghuna
+ menoni

(2 x 1 = alama 2)

(k) Huyo mwenyewe hakuzingatia funzo la lishe bora.

$4 \times \frac{1}{2} =$ (alama 2)

(l) Maana zifuatazo zijitokeze:

Gharama (i) jumla ya bei ya kufanyia jambo/pesa zinazohitajika kufanya jambo.

(ii) unalopoteza kwa kutozingatia maagizo.

Karama - kipawa kutoka kwa Mungu.

2 x 1 (alama 2)

(m) (i) Wanafunzi hawakuingia darasani wala hawakutoa vitabu wakaanza kusoma.
(ii) Wanafunzi hawakuingia darasani, wakatoa vitabu na kuanza kusoma.
(iii) Wanafunzi hawakuingia darasani na hawakutoa vitabu wakaanza kusoma.

2/0 - (alama 2)

(n) Nukta pacha
(i) Hutumiwa kutanguliza maneno halisi ya msemaji.
Mwalimu: Nawashauri msome kwa bidii.
Wanafunzi: Tunashukuru.
(ii) Hutumiwa kutanguliza maneno yaliyo kwenye orodha.
Alienda sokoni kununua: mapera, machungwa na papai.
(iii) Kutenga saa na dakika - saa 8 : 30
(iv) Kutenga shilingi na senti: Shilingi 10:50
(v) Kutenga sura na mstari, Yohana 8:30

2x1

(0) <u>**Wingu**</u> la nzige


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(p) Medali - nishani
Mchuano - Kinyang'anyiro, mchezo, mashindano, shindano, pigano.
(2 x 1 = alama 2)

(q) (i) Furaha - 1 - 1 (alama 1)
(ii) Nyasi - U - Z1/ Z1 (alama 1)

**Tanbihi**

Kuna baadhi ya watahiniwa ambao huenda wakatumia uainishaji wa ngeli unaozingatia viambishi awali vya nomino. Hawa pia watuzwe ipasavyo. Kwa mfano:

(i) Furaha - N - N
(ii) Nyasi - U - N / U - NY / N

(r) Mf

(i) Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi **licha ya** kukabiliwa na hatari.
(ii) **Pamoja na** hatari iliyowakabili, wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.
(iii) **Minghairi ya** kukabiliwa na hatari, wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

Mifano mingine: hata baada ya, ilhali, lakini, bali, bighari ya, ila

(s) **Majani ya mti huo** yalikatiwa ng'ombe wote na wafugaji.
Yambwa (tendwa) (alama 2)

4. (a) Kaida ambazo zinadhibiti sifa za lugha katika mazungumzo haya ni:

(i) Mada - uwekezaji
(ii) Umri / uhusiano - anawazungumzia vijana
(iii) Utungo - ni hotuba / mazungumzo ya moja kwa moja / ushauri - nasaha/ mawaidha
(iv) Muktadha - ni muktadha au hali rasmi kwani anatakiwa kutoa mazungumzo hayo.

Hoja zifuatazo zizingatiwe:

(i) Lugha rasmi - kuhusu uwekezaji.

(ii) Mtindo wa hotuba / mazungumzo ya moja kwa moja na hadhira / ushauri / mawaidha.

(iii) Msamiati au istilahi za kibiashara - unaohusu uwekezaji, kama vile biashara, hisa, faida, gharama. n.k.

(iv) Anaweza kutumia misimu ya vijana inapostahili ili kujinasibisha zaidi nao / kufanikisha mawasiliano.

(v) Kuchanganya ndimi, kwa mfano, kutumia Kiingeraza na Kiswahili; au hata *sheng* kwa kuiwekea mipaka pia.

(vi) Matumizi ya sentensi ndefu-ni hotuba / ushauri.

(vii) Anaweza kuishirikisha hadhira kwa kuiuliza maswali ya balagha, au kuwataka kutoa maoni.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(viii) Lugha elekezi - inayoshauri kuhusu njia chanya za uwekezaji. Hapa matumizi ya kauli au sentensi agizi yatatawala.

(ix) Lugha sanifu / lahaja sanifu itawale kwa vile huu ni utungo rasmi.

(x) Lugha inayotumia kauli shawishi ili kuwaonyesha umuhimu wa kuwekeza badala ya kutegemea ajira.

5 x 1 = 5

(b) (i) Msamiati wa kidini - kwa mfano, Jalali, Mungu, alleluia, amina.

(ii) Lugha chakavu / lugha ya kale, kwa mfano, sama badala ya mbingu.

(iii) Kunukuu vifungu kutoka kwenye msahafu - Biblia au Kurani ili kuwaaminisha waumini.

(iv) Lugha yenye toni kali ya kutisha hasa unapohubiri ili kukashifu tendo hasi.

(v) Lugha inayohimiza / inayoshawishi kutenda mema

(vi) Matumizi ya mafumbo, kwa mfano mbazi

(vii) Kurudiwa kwa vifungu fulani, kwa mfano Sala ya Bwana, Neema ya Bwana Yesu, amin.

(viii) Matumizi ya kweli kinzani / matumizi ya fantasia. Kusawiri mambo ambayo hayawezekani katika maisha ya kawaida.

(ix) Lugha inayoibusha mhemko / jadhba. Mfano, Amina, Amina

(x) Majibizano; kwa mfano: "Bwana awe nanyi - awe pia nawe"
"Bwana asifiwe - Amina"

(xi) Matumizi ya vihisishi au nidaa kama vile 'Ee', - ili kuibua hisia mbalimbali

(xii) Lugha inayojaza matumaini ya maisha mema. Mfano, 'kabla hujazaliwa nilikujua.'

(xiii) Lugha inayomhimiza binadamu kuwa mtegemezi kwa Mungu, k.v. "Msaada wangu unatoka kwa Mungu..."

(xiv) Lugha inayoyasawiri maisha ya binadamu kama yanayodhibitiwa na nguvu asizo na uwezo kwazo. Hana lolote la kufanya kuhusiana na maisha yake. Kwa mfano, "Hata ukahuzunika vipi huwezi kuongezea hata pima moja kwenye maisha yako."

(xv) Kuchanganya ndimi - hasa katika mahubiri.

(xvi) Mtumizi ya viziada - lugha kama vile ishara za mikono na uso, na miondoko ya mwili ili kuhuisha uhubiri.

(xvii) Lugha ya kushauri au kuelekeza. Kwa mfano, 'bisheni, nanyi mtafunguliwa.'

(xviii) Kutasfidi lugha ili kuondoa aibu. Kwa mfano, 'kujua mwanamke', badala ya kujamiiana.

5 x 1



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

### 4.2.3 Kiswahili Paper 3 (102/3)

1. (a)
   (i) Kauli ya kwanza ni ya Amani kwa Imani.
   (ii) Kauli ya pili ni ya Imani.
   (iii) Anamwambia Amani.
   (iv) Anamhadithia Amani kuhusu kadhia iliyompata; kupigwa kwa mama yake, kufa kwa mama yake, na kuchomewa nyumba, kisha kukashifu hali ya wanakijiji cha Baraka kutotenda lolote kumtetea.
   (v) Wamo kibandani mwa Amani.
   (vi) Imani anashangaa ni nani aliyewatuma askari kutekeleza matendo haya ya kinyama.

   4 x 1 = 4

   **Tanbihi**
   Dondoo limetolewa uk. 58.

(b)
   (i) **Kinaya** - mtu kufurahia msiba wa wengine.
   (ii) **Tanakuzi** - msiba na arusi ni vinyume - kuonyesha uovu/ugumu wa moyo.
   (iii) **Sitiari** - msiba - matatizo
   - arusi - furaha
   - mzigo wa mwenzio kanda la usufi - kudunisha matatizo ya wengine.
   - msiba kwa wengine kwake harusi - kufurahia matatizo ya wengine.
   (iv) **Methali**, "Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi", imedokezwa na kauli, 'Mzigo wa mwenzio kanda la usufi.'

   2 x 1 = 2

(c)
   (i) Raia wa Baraka, badala ya kumpoza Imani kwa kuchomewa nyumba, wanaogopa hata kuonekana wakizungumza naye, wanaaendelea tu na shughuli zao.
   (ii) Viongozi wanawadhulumu hata wasio na chochote. Nasaba Bora anawadhulumu akina Imani shamba lao na kujifaidi kwalo.
   (iii) Nasaba Bora anamuua Chichiri Hamadi ili kunyakua mali yake.
   (vi) Baadaye Yusufu anasingiziwa mauaji haya na anafungwa.
   (v) Nasaba Bora anampagaza Amani malezi ya Uhuru huku akijua mtoto si wa Amani. Hata anamtarajia Amani kuendelea na kazi yake ya uchungaji pamoja na ulezi huu.
   (vi) Nasaba Bora anashirikiana kimapenzi na msichana mchanga - Lowela - bila kujali mustakabali wake.
   (vii) Nasaba Bora anakitupa kitoto chake mlangoni pa Amani ili kujitoa lawamani bila kuwazia afya yacho.
   (viii) Nasaba Bora anamwachia mkewe upweke huku akitafuta raha kwa wasichana wadogo kama vile Lowela.
   (ix) Nasaba Bora anampiga Amani kikatili kwa shutuma zisizo na ithibati na kumtupa; anachojali ni kulipiza kisasi tu.
   (x) Fao anamwendea kinyume mwanafunzi wake kwa kuhusiana naye kimapenzi bila kujali unyonge wake kama mwanafunzi. Anapomtunga mimba anaondoka bila kujali hali ya mtoto na mama yake.
   (xi) Michelle anakataa posa ya Majununi hata baada ya Majununi kujikalifu kujenga jumba ili kutimiza masharti yake.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(xii) Majisifu anamwibia Amani mswada na kujifaidi kwao, hajali yatakayompata Amani.
(xiii) Majisifu, badala ya kuhudhuria madarasa, anaingilia ulevi bila kujali maendeleo ya wanafunzi wake.
(xiv) Wenzake Amani chuoni wanamsingizia uchochezi na kumfanya kufungwa na kukatiza masomo yake.
(xv) Nasaba Bora anawafungia Amani na Imani kwa madai kwamba wamekiua kitoto japo kimekufa kwa kichomi. Askari kuwabeza Amani na Imani.
(xvi) Wauguzi hospitali wanakosa kukitibu kitoto, wanasema ni sikukuu, hawafanyi kazi, na kusababisha kifo chacho, huku wakiendelea na shughuli zao.
(xvii) Serikali inawatelekeza wazalendo, kama vile Matuko Weye, hata anafungiwa anaposema ukweli kuwahusu viongozi.
(xviii) Nasaba Bora anamtaliki mkewe kwa shutuma ambazo hata hajathibitisha, licha ya kwamba mkewe amekuwa mwaminifu kwake. Yeye Nasaba Bora anaendelea na uhusiano wake na Lowela.
(xix) Serikali inawatelekeza wachezaji kama vile Makweche katika umaskini na ugonjwa hata baada ya kuiletea nchi sifa. Makweche anaishia kukatwa mguu.
(xx) Askari wanampiga mamake Imani machoni pake bila kujali dhiki ya kisaikolojia wanayomsababishia. Baadaye Mama Imani anakufa kwa maumivu haya.
(xxi) Oscar Kambona, baada ya kuuawa kwa mama yake, anaondoka bila kuaga, anamwachia Imani ukiwa.
(xxii) Wahudumu katika zahanati hawamshughulikii DJ. DJ analazimika kuondoka hospitali kutafuta matibabu kwingine.
(xxiii) Serikali, badala ya kufadhili elimu ya maskini, inatumia pesa hizi kudhamini elimu ya wanaojiweza kama vile Fao. Fao anapelekwa kusomea ng'ambo.
(xxiv) Nasaba Bora anawashurutisha raia kuchangia elimu ya mwanawe - Madhubuti, hajali hali yao duni kiuchumi. Madhubuti anakwenda kusomea Urusi.
(xxv) Majisifu anawadharau wanawe wenye mahitaji maalum. Anamwachia mkewe ulezi bila kujali dhiki anazomsababishia. Hawapeleki wanawe shuleni au kwa uangalizi maalum.
(xxvi) Nasaba Bora, badala ya kuwahudumia raia katika afisi za Wizara ya Ardhi anaficha faili na kuwalazimisha kutoa hongo ili kuhudumiwa.
(xxvii) Nasaba Bora hajali afya ya majibwa yake, hayachanji.
(xxviii) Nasaba Bora anawafuta wafanyakazi wake kiholela, hata kwa kunadhifisha maskani yake, hajali watapata wapi riziki.
(xxix) DJ kuumwa na jibwa na mtemi hajali.
(xxx) Mtemi kumpita mama anayejifungulia njiani huku mvua ikinyesha. Hajali kumsaidia hata anaponasihiwa na mkewe.
(xxxi) Wazungu kunyakua mashamba ya Waafrika.
(xxxii) Wazungu kuwakataza Waafrika kufuga na kupanda baadhi ya mimea.
(xxxiii) Mashaka kuwabeza watoto walemavu wa Majisifu.
(xxxiv) Majisifu anaposhindwa kutoa mhadhara wanafunzi wanamcheka /wanamkejeli.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

**Tanbihi**

(i) Mtahiniwa anaweza kuonyesha:

Tendo la kikatili linaloelekezwa kwa mhusika au kundi fulani, kwa faida ya anayetenda tendo hilo,

**Au**

Aonyeshe hali ya mapuuza au dhuluma inayosababisha kuhasirika kwa mwingine.

(ii) Si **lazima** anayetenda tendo hilo la kikatili afaidike moja kwa moja. Mtahiniwa anaweza kujadili tu namna mhusika anavyomdhulumu mwingine **bila kujali**, au kuwazia uchungu anaomsababishia.

7 x 2 = 14

2. (a) (i) Ni maneno ya Diwani I.

(ii) Anamwaambia Meya, Diwani II na Diwani III.

(iii) Wamo ofisini mwa Meya.

(iv) Meya amewaita ili kutafuta njia ya kuwadhibiti watu ambao anadai wamechochewa na baadhi ya madiwani kulalamikia hali ya Baraza kushindwa kutimiza majukumu yake.

(v) Meya anawauliza wafanye nini, ndipo wanaanza kutoa maoni, na Diwani I kusema haya.

4 x 1

**Tanbihi**
Dondoo limetolewa Uk. 21.

(b) Matumizi ya vitisho. Diwani I anasema watakaogoma watafutwa.

**Au**

Kuwanyanyasa/kuwaangamiza wanaotetea haki - Diwani anataka kuwadhibiti wafanyakazi kwa kuwafuta.

(c) (i) **Hila/udanganyifu/unafiki.** Meya anamwambia Siki kwamba ana akili, ndio maana watu wakamchagua, Meya anaahidi dawa ambazo hazimo, ili watu watulie.

(ii) **Uteuzi wa washauri ambao ni vibarakala wa Meya.** Diwani I anasema kwamba jukumu lao ni kuhakikisha wamelilinda Baraza la Mstahiki Meya, kwamba wanalipwa kwa sababu hii.



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(iii) (a) **Propaganda** - kuwatangazia kujitolea kwa Baraza kutetea demokrasia, na hali sivyo.

(b) Mashindano kupeperushwa moja kwa moja kupitia vyombo vya habari ili kuibua hisia za uzalendo.

(iv) **Uundaji wa kamati za kuhudumu** (za madiwani).
Madiwani wenye ushawishi mkubwa wanateuliwa kuongoza kamati hizi ili kusiwe na upinzani. Meya hajali pesa zitakazotumiwa kuendesha kamati hizi.

(v) **Hongo/vishawishi.** Meya anaidhinisha nyongeza ya mishahara ya madiwani na kutotozwa kodi kwao ili wamuunge mkono.

(vi) **Meya anakabiliana na migomo ya wafanyakazi kikatili (kupigwa)**. Askari wanawatawanya wafanyakazi waliogoma.

(vii) **Dini** - Mhubiri anahongwa ili kumuunga mkono.

(viii) **Kuunda sheria ambayo inampa Meya mamlaka makubwa yanayomfanya kuongoza kwa mabavu.** *Mayors Act* inampa mamlaka ya kumnyamazisha yeyote anayempinga. Meya ndiye mwenye mamlaka juu ya ugavi wa viwanja vya umma, hivyo anaufisidi uchumi wa Cheneo kwa kujigawia viwanja na kumgawia Bili pia.

(ix) **Kuwatenga washauri/viongozi wanaompinga Meya.** Maamuzi yanayohusiana na matumizi ya pesa yanatolewa na Meya, Diwani I, Diwani II huku wanamtenga Diwani III ambaye ndiye kinara wa masuala ya fedha. Kwa njia hii Meya anaweza kutoa maamuzi yanayomfaa yeye na vikaragosi wake bila pingamizi.

(x) **Kujilinganisha na mataifa dhaifu kiuchumi ili kuonekana na raia kwamba wameendelea.** Meya anasema kwamba Cheneo ni kisiwa chenye amani, huku Siki akimwonya dhidi ya kujilinganisha na chumi dhaifu.

7 x 2 = 14

3. (i) Wagonjwa wanaambiwa wangojee dawa zilizoangizwa, ambazo kwa kweli hazijaagizwa baadhi wanaishia kufa - yule mtoto (Dadavuo).

(ii) Kutoshughulikiwa kwa mishahara duni ya wafanyakazi na kutoboreshwa kwa hali yao ya maisha na utendakazi kunasababisha mgomo wa wafanyakazi.

(iii) Malimbikizo ya mishahara yanawafanya wafanyakazi kukata tamaa, na baadhi yao, kwa mfano Waridi, wanajiuzulu, wengine wanagoma.

(iv) Kutoboreshwa kwa maisha ya wafanyikazi kunawafanya kuishi maisha yasiyo na hadhi. Wanakula makombo (yaliyoharibika) kwa waajiri. (mf. Mama mtoto).

(v) Wafanyakazi wanakosa vifaa vya kufanyia kazi. Wanadai subira yao imeisha. Mji unaenea uchafu.

(vi) Wafanyakazi wanaposita kuzoa taka mji unarundikana uchafu. Uvundo unaenea hadi afisini mwa Meya.

(vii) Kurundikana kwa uchafu, na tishio la mkurupuko wa magonjwa unawafanya wageni kutozuru Cheneo. Meya anaaibika.

(viii) Meya anapuuza ushauri wa Diwani III kuhusu matumizi ya fedha na kulisababishia Baraza nakisi ya pesa/ Siki kumshauri Meya mara kwa mara na ushauri kupuuzwa.

(ix) Meya anakosa kuona udanganyifu wa Bili, anaishia kusababisha kuibwa kwa fimbo yake mwenyewe ambayo ndiyo kiwakilishi cha umeya.

(x) Raia wanapuuza umuhimu wa kuwachagua viongozi waadilifu. Wanawachagua viongozi dhalimu na kurithisha uongozi mbaya kwa kuwachagua wabaya wakijua tu ni wabaya.



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(xi) Wanataaluma wanakataa kuingia katika siasa (mf. Siki), nchi inakosa huduma yao, uongozi mbaya unaendelezwa zaidi.

(xii) Meya anapuuza mpango wa maendeleo wa miaka kumi (wa mji), akidai wao wanathamini malengo ya kimilenia. Cheneo inashindwa kuzua mipango ya kuzalisha pesa/pato la kuongezea mishahara ya wafanyakazi.

(xiii) Meya anakosa kudhibiti tamaa yake, anamruhusu Bili kumshawishi kulipagaza Baraza deni kupitia ile kesi ya mwanakandarasi. Meya anafaidika huku uchumi wa Cheneo ukidorora.

(xiv) Meya anashindwa kuurekebisha uongozi wake licha ya ushauri wa Siki na Diwani III. Anaupujua (anaudhoofisha) uongozi wake, na kuishia kung'olewa uongozini.

(xv) Meya anashawishiwa na Diwani I na II kuunda kamati nyingi, **hawazii umuhimu** wa kamati hizo. Anaishia kuifilisi hazina ya baraza.

(xvi) Kutodhibiti mgomo wa wafanyakazi kwa kushughulikia malalamishi yao kunasababisha kutokusanywa kwa kodi, Baraza linapoteza fedha.

(xvii) Baraza linashindwa kudhibiti usalama mjini. Askari wameutwaa mji. Wanawafukuza wafanyakazi, wanawafanya watu kukaa tu nyumbani, kutazama matukio yanavyoendelea (Mfano Diwani III).

(xviii) Meya anapuuza umuhimu wa madiwani kulipa kodi na kusababisha kuzorota kwa pato la Baraza.

(xix) Meya, badala ya kuzalisha pesa kulipia mishahara, anategemea kuzipata kutoka kwa wafadhili/washirika wao wa kimaendeleo. Hawazi kuwa huu ni mzigo anaovirithisha vizazi vya kesho. Anapalilia hali ya utegemezi.

(xx) Hali ya baadhi ya wanyonge kujiwazia wao wenyewe inafanya hali ya jamii ya wanyonge kutobadilika. Dida anasema kwamba hajali hali ya Meya kuwapeleka watu wake mbali na uvundo wa mji, mradi mameya waendelee kuwepo naye aendelee na kazi yake duni ya kunadhifisha nyumba zao.

(xxi) Meya anapuuza umuhimu wa kutumia pesa za umma vyema. Anabadhiri pesa kwa kumpeleka Bili kujistarehesha na kumpeleka mkewe kuzalia ng'ambo.

(xxii) Meya, anaendeleza hali duni ya elimu, badala ya kuiboresha, anawapeleka wanawe kusomea ng'ambo.

(xxiii) Meya anapuuza athari za mgomo wa wafanyakazi/anapuuza umuhimu wa wafanyakazi wa kima cha chini. Anamwambia Diwani III kwamba hata wakigoma, watarudi baada ya siku chache; kwamba mahitaji ya kimsingi yatawasukuma kurudi kazini. Hili linaathiri utendakazi wa Baraza, pia linasababisha kuong'olewa mamlakani kwake.

(xxiv) Meya anakataa kushughulikia changamoto za leo. Anasema kesho ... na mtondogoo hawatakuwepo, hivyo haina haja kujidhiki. Mtazamo huu wake ndio unaofanya uozo Cheneo kuongezeka, na kuangamia kwa uongozi wake.

(xxv) Badala ya Meya kuhifadhi hazina ya Baraza, anaifilisi zaidi kwa kumpa mhubiri sadaka ya elfu mia moja kila mwezi.

(xxvi) Meya anaongozwa na **mtazamo finyu** kulifilisi Baraza zaidi kwa **kuagiza** hata mvinyo wa kuwastareheshea wageni kutoka ng'ambo. Anatumia pesa hizohizo wanazoleta kwa manufaa ya hao hao wageni.

(xxvii) Meya anapuuza wajibu wake wa kuilinda ardhi ya Cheneo; anajigawia ardhi na kumgawia Bili. Anaendeleza zaidi ukiukaji wa sheria kuhusiana na ugavi wa ardhi.

**Tanbihi**



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

Mtahiniwa **sharti** aonyeshe pande **mbili**.

(i) Kupuuza/kungojea /kutoshughulikia/kukaidi/kutoona hila, au hasara/kufuja/kubadhiri.
(ii) Kuhasirika/kuzorotesha hali zaidi/kutofanikiwa/kuangamia kwa uongozi.

10 x 2 = 20

Kutoshughulika/kupuuza/kudhulumu -1
Hasara/athari mbaya - 1

4. (a) (i) Ni maneno ya Babu/Babu Maende/Maende.
(ii) Anamwambia mjukuu wake/msimulizi.
(iii) Wamo mtaa wa Madongo/wamo Kochokocho sehemu iitwayo Madongo.
(iv) Babu ameona hali duni/majengo duni yaliyosongamana hapa, ndipo akasema haya/Babu amewaona wanawake wanaokaanga samaki na kuwauzia wapita njia katika kitongoji hiki duni, ndipo akasema haya.

4 x 1 = 4

**Tanbihi**
Dondoo limetolewa Uk. 78

(a)(II) (i) Anadhihirisha/anahimiza umuhimu wa raia kuendeleza sehemu za mashambani badala ya kujidhiki kwa maisha duni mjini yanayopalilia umaskini zaidi. (Uk. 78)
(ii) Anaonyesha hali ya kukatisha tamaa mjini. (Uk. 78).
(iii) Anaendeleza maudhui ya usaliti. Anasema kwamba alidhani uhuru wa Sakata utaleta manufaa kwa wote, ila sivyo. (Uk. 78).
(iv) Anakashifu ubaguzi kwa misingi ya utabaka/anakashifu utabaka. Anasema Sakata ina makabila mawili tu; maskini na tajiri.
(v) Ni kielelezo cha wazalendo wanaopinga ukabila. Kila mara aliwazungumzia wanawe kuhusu ukabila Sakata.
(vi) Anadhihirisha na kupinga ufisadi nchini Sakata.
(vii) Anamjuza msimulizi akiwa mchanga kuhusu hali halisi katika jamii yake. Msimulizi alimsikia babu akitaja maneno kama vile uhuru, ukabila, hongo, ufisadi. (Uk. 78).
(viii) Anaendeleza mshikamano wa kijamii kwa kumkubalia mwanawe kuoa mke asiyetoka kwenye jamii yao.
(ix) Ni kielelezo cha mwanajamii mwenye bidii. Hapendi kuiacha mifugo yake kuja mjini, anakuja mjini tu kwa shinikizo la mwanawe.
(x) Anaonyesha ukiukaji wa haki za kibinadamu. Umati unampiga na kumuua kwa tuhuma kuwa ni mwizi wa watoto.
(xi) Kupitia kwake tunasawiriwa uozo katika jamii ya Sakata. Wizi wa watoto unaendelezwa.
(xii) Anaonyesha madhara/hatima ya ubaguzi wa rangi. Anauawa kwa tuhuma kwamba ameiba mtoto kwa vile mtoto ana rangi tofauti na yake.
(xiii) Kupitia kwake tunaona ukakamavu wa msimulizi - anamuuma mama aliyempiga Babu ili kumtetea.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

8 x 1 = 8

(b) (i) **Kinaya**

Ni kinaya kwamba mchuuzi anamsihi msimulizi/Christine awakumbuke watoto na kuwaonea huruma na hali Christine amekwisha kuavya mimba.

1 x 2 = 1
Kutaja 1
Maelezo 1

**AU**

Kejeli/stihizai/dhihaka

Mchuuzi anamdhihaki Christine kwa kumwomba awaonee watoto huruma na hali Christine ameavya mimba.

(ii) (a) Ni kinaya kwamba wavuvi wanasagika kuvua na faida inamwendea Peter.

(b) Ni kinaya kwamba Diogracias anawadharau akina Christine na hali ni Waafrika wenzake. Anawazungumzia Kiganda ili kuwadhalilisha.

(c) Christine anadai kwamba ameokoka na hali anahusiana kimapenzi na Peter.

(d) Dorothy, ambaye anasema ameokoka hamwambii Christine moja kwa moja akome kuhusiana kimapenzi na Peter.

(e) Ni kinaya kwamba Peter ana mazoea ya kulalamikia hali duni Afrika na hali yeye anatoka kwenye tabaka duni huko kwao.

(f) Muuguzi Margaret na Miriam, badala ya kumkataza Christine kuavya mimba, wanamwacha tu aavye.

(g) Mchuuzi anamtaka Christine kuwanunulia watoto peremende na hali Christine ameavya mtoto wake. Hii ni njia ya kuukejeli ukatili wa Christine.

(h) Peter, badala ya kuhuzunika kwa tendo la uavyaji mimba, anatabasamu tu, na baadaye kumuuliza Christine iwapo anataka pesa.

**Tanbihi**

Hoja kuhusu kejeli zinaweza kuingiliana na kinaya, mradi mtahiniwa aonyeshe kauli inavyodhamiriwa kumuumiza anayelengwa.

3 x 2 = 6

5 (i) Jamila hajaridhika - Duni analewa kupindukia - hata lakabu yake - Duni inahalalishwa na ulevi huu.

(ii) Hajaridhika kwa kuaibishwa na Duni anaporudi kijijini akiimba na kuwaghasi wakazi wa mtaa wa Sebleni.

(iii) Ukaidi na dharau ya Duni hairidhishi. Anakanywa na wanakijiji dhidi ya ‘taarabu - njia’ lakini anakataa.

(iv) Wanasebleni wamemtoa Duni maanani, wanamwona kuwa hana thamani mbele ya madebe ya taka. Hili haliwezi kuridhisha.

(v) Jamila anatiwa wasiwasi na tabia ya Duni. Pamoja na umri wake mbichi anamsubiri Duni usiku kwenye roshani.

(vi) Duni anamliza Jamila. Jamila hata anatamani ingekuwa mara ya mwisho kusikia wimbo wa Duni. Duni hajutii matendo yake mabaya kwa mke wake.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover Learn Apply

(vii) Duni anampiga Jamila na hata kumpa majeraha na makovu ya mwili.
(viii) Duni anamtusi na kumsimbulila Jamila.
(ix) Jamila hajaridhika kwani ana mgogoro wa nafsi. Anawaza ikiwa aufuate ushauri wa wanaomnasihi kutoka kwenye ndoa yenye utesi au abaki. Anaamua kutousaliti moyo wake. /Hata Salim, shangazi wanamsihi atoroke.
(x) Hisia/matukio ya Duni hayawezi kutabirika. Jamila anapojaribu kumsaidia anamwambia amwache, hahitaji msaada; inabidi Jamila akubali kuwa Duni hahitaji msaada; anaweza kila kitu.
(xi) Duni anamhangaisha Jamila kwa kumtaka Jamila kuleta chakula haraka japo kwa kweli Duni hakili chakula hicho.
(xii) Duni amemuumbua Jamila. Tunaambiwa Jamila hana tena lile busu la Zamani, anaonekana mwenye simanzi hata akiwa usingizini.
(xiii) Jamila ana dhiki ya kisaikolojia. Usingizi wake ni wa machovu.
(xiv) Jamila anaishi kwa hofu ya kuchelea kuvunjika kwa ndoa yake na Duni. Anatumainia kuwa siku moja Duni atabadilika.
(xv) Duni anarudi nyumbani usiku mkuu saa saba unusu/kuchelewa.
(xvi) Duni anawatusi wakazi wa mtaa wake, hivyo tabia hii haiwezi kumridhisha mkewe.
(xvii) Duni anamwaibisha Jamila hata kwa majirani; majirani wanasikia matusi anayomwaiwa na mumewe.
(xviii) Jamila analazimika kujitia bashasha pale Duni anaporejea akiwa mlevi ili kumridhia mumewe.
(xix) Duni analala akiwa amevaa nguo alizoshindia ulevini.
(xx) Maneno ya Duni ya kinyume yanamsumbua Jamila. Anamwambia awaambie watu ameridhika na hali hajaridhika. Hata Duni mwenyewe anasema kwamba penzi lina miujiza, kuonyesha kwamba yeye ana udhaifu mkubwa na hata Jamila ana udhaifu kwa kuishi naye. (Uk. 57).

10 x 2 = 20

6. (a) (i) Shairi linazungumzia tatizo la upofu.
Mf. ngakua na mato.

(ii) Kwamba mtu aliyepatwa na tatizo la upofu huwa hawezi kufanya mambo ambayo zamani aliyamudu bila tatizo.

**AU**

Nafsineni inasikitikia hali yake ya kutomudu kujifanyia mambo kwa sababu ya upofu.

1 x 2 = 2
Kutaja - 1
Mfano - 1

(b) (i) Inkisari - imetumika ili kudumisha ulinganifu wa mizani.

Mifano:

| | | |
|---|---|---|
| ngaliandaa | - | ningaliandaa |
| ngafinyanga | - | ningalifinyanga/ningefinyanga |
| ngatia | - | ningetia |

Tabdila - imetumiwa ili kuleta urari wa vina



Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

mduwaa - mduara
apikae - apikaye
vinavong'aa - vinavyong'aa
kuupa utungo mahadhi ya kishairi

2 x 2 = 4
Kutaja - 1
Sababu - 1

(c) Ningetumia miti iliyopinda (iliyokatika) na yenye umbo zuri kutengenezea kijiti (ulindi). Ningekipekechea kijiti hiki kwenye tundu la wimbombo mwema/mzuri kupekechea moto kwa ufundi/umahiri mkuu kiwamboni. Ningekuwa bingwa/ ningekuwa na moyo mahiri/shupavu (katika upekechaji) na kupekecha moto/ Ningekuwa fundi stadi katika upekechaji wa moto.

4 x 1 = 4

**Tanbihi**

(i) **Wimbombo** - kipande cha mti kilichotobolewa tundu, na kinachotumiwa kupekechea moto.

(ii) **Ulindi** - Ni kijiti kinachopekechwa kwenye wimbombo ili kutoa moto.

(d) Toni ya huzuni/toni ya kuomboleza/ya masikitiko.
Mshairi anahuzunishwa na analalamikia hali yake ya upofu isiyomruhusu kujifanyia mambo mengi.

Kutaja - 1
Maelezo - 1

(e) (i) Urudiaji wa sauti/silabi.
Kwa mfano ubeti wa kwanza: to, to, to / a, a, a
Mstari wa mwisho wa kila ubeti - e

(ii) Urudiaji wa maneno, kwa mfano, ulo - ubeti wa 3.

(iii) Usambamba/urudiaji wa vishazi/urudiaji wa miundo sawa ya mistari.
kwa mfano,
ngalisana kito, cha kuchezea
ngafinyanga chungu, cha mduwaa

3 x 2 = 6
Kutaja - alama 1
mfano - alama 1

(f) Nafsineni ni kipofu/mtu asiyeona. Ubeti I anasema, 'ngakua na mato!'Ubeti 9 anasema, 'mato ndo malenga kanikimbia'.

Alama2
Kutaja - alama 1
mfano - alama 1

7. (i) Hodari wa kufanya kazi/wenye bidii/hodari.


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(ii) Wenye kujiamini
(iii) Waliopuuzwa/hawana makubwa (hawasikiki)
(iv) Hawana tamaa
(v) Wenye kupinga ulaghai
(vi) Wenye matumaini/ndoto haizimiki.
(vii) Hawahini/huwapa watu haki yao.
(viii) Wanahakikisha kuwa jamii imejitosheleza kwa chakula/hawatulii hadi wapate.
(ix) Wazalendo

5 x 1 = 5

(i) Tashbihi - kama watanga na mipini - kuonyesha jinsi walivyojitolea.
(ii) Tashihisi/uhaishaji
Tamaa za moyo kutii, kupigana na ulaghai. Hapa tamaa za moyo na ulaghai vimepewa uwezo wa kutenda. Binadamu anasawiriwa kama aliye chini ya mamlaka ya tamaa za moyo ambazo ndizo zinazotiiwa. Pia ulaghai unapewa uwezo wa kukabiliana ana kwa ana na binadamu. Imetumiwa kuonyesha ugumu uliopo wa kujitenga na tamaa na ulaghai.

(iii) Nahau/msemo - ndoto haizimiki. Hawapotezi tumaini, kuonyesha hali ya kutokata tamaa

La haramu jasho hawali - Kuonyesha hawafaidiki kwa wasichokifanyia kazi.

(iv) Hisi mseto.
Ndoto haizimiki, na jasho hawali.
Hapa tendo au jambo linalohusiana na kuona (haizimiki) linahusishwa na jambo au hisi ya kuonja/muonjo (kula - jasho hawali).

(v) Taswira.
'Kutwa kile na hiki, kama watanga na njia - kuonyesha watu wanaoshughulika kufanya kazi kuiendeleza nchi.

(vi) Sitiari/jazanda - ndoto haizimiki - hawapotezi tumaini - kuonyesha kujibidiisha kwa watafuta riziki.

3 x 2 = 6
Kutaja - 1
umuhimu - 1

(c) (i) Mazida - vinyuani badala ya vinywani - ili kutosheleza mahitaji ya idadi ya mizani.
(ii) Kufinyanga sarufi//kuboronga lugha/miundo ngeu/ukiushi wa kisintaksia/ ukiushi wa kimuundo.

Mifano


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

(i) Tamaa za moyo kutii, badala ya, Kutii tamaa za moyo.
(ii) La haramu jasho hawali - badala ya, 'hawali jasho la haramu'.
(iii) Ya kesho kuwa hali njema, badala ya, ya hali kesho kuwa njema.
Imetumiwa ili kupata urari wa vina.

(iii) Udondoshaji wa maneno, mfano,

(i) Pato ambalo la halali - badala ya, Pato ambalo ni la halali.
(ii) Wiki baada wiki - Wiki baada ya wiki.
Umetumiwa ili kutosheleza idadi ya mizani / kupunguza idadi ya mizani.

3 x 2 = 6 Kutaja - 1
Mfano - 1

(d) (i) Tathlitha - Mishororo mitatu katika kila ubeti.
(ii) Ukara - Vina vya kati / ndani vinafanana katika shairi zima, vya nje vinatofautiana
(iii) Kikwamba - kila ubeti unaanza kwa kirai / maneno, "Watafuta riziki".

3 x 1

8. (a) (i) Kisasili / kisasili cha usuli.
Inazungumzia asili ya kifo.

alama 2

(ii) (a) Hutumiwa kuelezea chanzo cha mazoea ya kidini/kijamii. Kwa mfano asili ya dhehebu fulani, asili ya kifo.
(b) Ni tungo zinazohalalisha baadhi ya desturi na imani za kidini za jamii.
(c) Ni kitambulisho cha jamii. Kila jamii ina kisasili au visasili vyake vinavyohusu imani zayo.
(d) Hurithisha imani, desturi, na historia ya jamii kwa kuvitamba kwa vizazi mbalimbali.
(e) Ni nyenzo ya kuadilisha. Kila kisasili huwa na adili. Kwa mfano, kisasili cha hapo juu kinafunza haja ya kutandarukia mambo.
(f) Huimarisha utangamano wa kijamii. Watu wanapokuja pamoja kutambiana hujihisi kuwa kundi moja, hivyo umoja kujengeka zaidi.
(g) Hadithi hizi hutumiwa kupunguza athari za baadhi ya mambo ya kimaumbile au misiba inayompata binadamu. Kwa mfano, kisasili kuhusu chanzo cha kifo hunuiwa kuwapunguzia wanajamii mwemeo wa huzuni, binadamu hulazimika kuwaza kuwa kifo kilihalalishwa na matendo ya binadamu mwenyewe, hivyo hakiepukiki.
(h) Huburudisha. Watu wanapotambiwa huburudika na kuliwazika.
(i) Utambaji wa visasili hurithisha fani yenyewe ya utambaji kwa vizazi mbalimbali.
(j) Hukuza ubunifu. Kadiri mtu anavyotamba, ndivyo anavyopalilia kipawa cha kubuni mitindo ya kuisimulia hadithi.
(k) Hukuza ukakamavu wa kuzungumza hadharani. Kadiri mtu anavyotamba ndivyo anavyopalilia ujasiri wa kuzungumza hadharani.
l) Ni njia ya kudhibiti matendo hasi ya wanajamii. Baadhi ya visasili huhadithia maeneo matakatifu kama vile madhabahu,


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

Watu huelekezwa kuheshimu mahali hapa.

m) Hutumiwa kupitisha muda. Watu hushiriki vikao vya utambaji wakingojea shughuli nyingine kama vile kuiva kwa chakula.

(n) Kukuza lugha.

5 x 2 = 10
Kutaja - 1
Kufafanua / Kutoa mifano - 1

**Tanbihi**

(i) Mtahiniwa **lazima** afafanue hoja ili kupata **alama 2**.
Kutaja, kwa mfano, 'visasili huburudisha,' bila kuelezea vipi, hakutoshi.
Mtahiniwa huyu atuzwe alama 1.

(ii) Visasili **ni tofauti** na ngano za **usuli**. Ngano za usuli hazihusiani na imani za kidini. Atakayesema kwamba utungo huu ni ngano ya usuli apate **0** kote kote, (i) na (ii).

(b) Fomyula ya kumalizia

(i) Huonyesha kumalizika kwa ngano, hivyo kufunga muktadha wa ulimwengu wa usimulizi/ulimwengu usio halisia.
(ii) Hapa ndipo fanani hutangaza Adili au funzo la usimulizi wake. Kwa mfano, mtambaji anaweza kusema, "mwenye kujaribu kuokoa maisha ya binadamu mwenzake na afuatwe na utajiri, na mwenye kuyaangamiza agubikwe na umaskini", ili kuonya dhidi ya kumdhulumu mwenzako maisha.
(iii) Baadhi huwapa wasikilizaji changamoto ya kuwa watambaji bora, hivyo kurithisha stadi bora za utambaji.
(iv) Humpisha mtambaji anayefuata. Anaweza kuashiriwa kwa kauli fulani au kwa kupewa changamoto.
(v) Huitoa hadhira kwenye ulimwengu wa ubunifu na kuaingiza kwenye ulimwengu halisia, hivyo kupunguza makini yao.
(vi) Hupisha shughuli inayofuata, (kwa mfano utegaji wa vitendawili) iwapo shughuli ya utambaji imekwisha.
(vii) Hutuliza hadhira, pengine kwa kuipa suluhisho kwa mgogoro uliopo kwenye ngano. Kwa mfano, inaweza kuonyesha kuuawa kwa zimwi na kurejeshwa kwa usalama katika jamii fulani.
(viii) Hutia mshawasha wa kusikiliza ngano nyingine; pengine kupitia taharuki ambayo huenda ikaibuliwa na fanani, au kukatizwa kwa msuko wa ngano yenyewe.

4 x 2 = 8
Kutaja - 1
Kueleza - 1


Powered by: www.manyamfranchise.com
MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply